



Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Simu: +255 (0)22-2122722/3
Nukushi: +255 (0)22-2130852
Barua pepe: dg@nbs.go.tz
Tovuti: www.nbs.go.tz

18 Barabara ya Kivukoni,
S.L.P. 796,
11992 - Dar es Salaam
TANZANIA.



Unapojibu tafadhali taja:
Kumb Na: NBS/S.40/21/520

YALIYOJITOKEZA

Tarehe: 09 Januari, 2017

FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA KWA MWEZI DESEMBA, 2016

MAELEZO YA MBINU NA KANUNI ZA UKOKOTOAJI FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA

Maana ya Fahirisi za Bei za Taifa

Fahirisi za Bei za Taifa ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumiwa na sampuli wakilishi ya kaya binafsi nchini Tanzania. Bei za bidhaa na huduma 278 zikiwa ni pamoja na bidhaa 97 za Vyakula na Vinywaji Baridi na 181 zisizo za Vyakula hukusanywa kila mwezi katika kila mkoa.

Mizania Mpya za Bidhaa na Huduma na Jamii na Kizio cha Bei

Mizania ya Fahirisi za bei za Taifa zimetokana na matumizi ya kaya binafsi kutoka mikoa 25 ya Tanzania Bara. Mizania inajumuisha matumizi ya kaya zote binafsi kutoka mijini na vijijini yaliyotokana na Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya binafsi wa mwaka 2011/12. Kizio cha bei kinachotumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa ni cha mwezi Desemba, 2015.

Makundi ya bidhaa na huduma za jamii

Marejeo ya Fahirisi za Bei za Taifa yamefanyika kwa kufuata makundi yaliyokubalika Kimataifa yanayoitwa mchanganuo wa matumizi binafsi "Classification of Individual Consumption by Purpose (COICOP)". Fahirisi mpya za Bei inajumuisha makundi 12 ya mfumo wa COICOP pamoja na fahirisi za bei kwa makundi maalumu. Makundi hayo maalumu ni; 1) Vyakula na vinywaji baridi-vikijumuisha vyakula vinavyoliwa majumbani na mahotelini; 2) Nishati na Mafuta - kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli; 3) Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi; 4) Fahirisi za huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, vinywaji baridi, nishati na mafuta.

Namna ya kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa

Kuna maboresho mengi yamefanyika kwenye ukokotoaji wa Fahirisi mpya za Bei za Taifa ikiwa ni pamoja na kutumia wastani wa jiometa "geometric mean of Price Relatives" kwenye kukokotoa Fahirisi za Bei katika ngazi za mwanzo; matumizi ya mfumo ulioboreshwa wa ukokotoaji pamoja na mfumo mzima wa kukusanya na kuchambua bei. Mbinu na kanuni ya Lowe Index Formula ambayo ni aina ya "Laspeyres Index Formula" inaendelea kutumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi ya makundi makubwa.

MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWAKA UMEONGEZEKA HADI ASILIMIA 5.0

Jedwali Namba 1: Badiliko la Fahirisi za Bei za Taifa kwa Mwezi Desemba, 2016 (Des., 2015 = 100)

Na .	KUNDI (MAIN GROUP)	Mizania (Weight)	Des-15	Nov-16	Des-16	Badiliko la mwezi mmoja	Badiliko la miezi 12
1	Vyakula na vinywaji baridi	38.5	100.00	105.25	106.95	1.6	7.0
2	Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku	3.7	100.00	104.99	105.11	0.1	5.1
3	Mavazi ya nguo na viatu	8.3	100.00	103.27	103.72	0.4	3.7
4	Nishati, Maji na Makazi	11.6	100.00	110.58	109.93	-0.6	9.9
5	Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba	6.3	100.00	103.15	103.98	0.8	4.0
6	Gharama za Afya	2.9	100.00	104.59	104.72	0.1	4.7
7	Usafirishaji	12.5	100.00	100.00	100.32	0.3	0.3
8	Mawasiliano	5.6	100.00	99.05	99.09	0.0	-0.9
9	Utamaduni na Burudani	1.6	100.00	101.72	101.84	0.1	1.8
10	Elimu	1.5	100.00	102.64	102.64	0.0	2.6
11	Hoteli na Migahawa	4.2	100.00	104.23	104.24	0.0	4.2
12	Bidhaa na huduma nyinginezo	3.1	100.00	102.74	102.86	0.1	2.9
JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE		100.00	100.00	104.32	105.04	0.7	5.0
Makundi Mengine Teule							
1	Vyakula—vikijumuisha vyakula vilivyoliwa nyumbani na mahotelini	37.07	100.00	105.68	107.44	1.7	7.4
2	Nishati na Mafuta—kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika nyumbani pamoja na petroli na dizeli	8.68	100.00	111.94	111.66	-0.2	11.7
3	Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula	62.93	100.00	103.65	103.77	0.1	3.8
4	Fahirisi na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, nishati na mafuta	54.25	100.00	102.33	102.51	0.2	2.5

Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa kipimo cha mwaka unapima kiwango cha kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Jedwali Namba 1 hapo juu linaonesha kuwa, Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa mwezi Desemba, 2016 umeongezeka hadi kufikia asilimia 5.0 kutoka asilimia 4.8 mwezi Novemba, 2016. Hii inamaanisha kuwa, kasi ya upandaji wa bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia mwezi Desemba, 2016 imeongezeka ikilinganishwa na kasi ya upandaji ilivyokuwa kwa mwaka ulioishia mwezi Novemba, 2016. Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 105.04 mwezi Desemba, 2016 kutoka 100.00 mwezi Desemba, 2015. Mfumuko wa Bei wa bidhaa za Vyakula na Vinywaji Baridi kwa mwezi Desemba, 2016 umeongezeka hadi asilimia 7.0 kutoka asilimia 6.2 ilivyokuwa mwezi Novemba, 2016.

Mfumuko wa Bei kwa Bidhaa za Vyakula na Bidhaa Zisizo za Vyakula


Mfumuko wa Bei kwa kipimo cha mwaka wa bidhaa za vyakula nyumbani na migahawani kwa mwezi Desemba, 2016 umeongezeka hadi asilimia 7.4 kutoka asilimia 6.4 mwezi Novemba, 2016. Aidha, badiliko la Fahirisi za Bei kwa bidhaa zisizo za vyakula limebaki katika asilimia 3.8 mwezi Desemba, 2016 kama ilivyokuwa mwezi Novemba, 2016.

Mfumuko wa Bei wa Bidhaa na Huduma zote Isipokuwa Bidhaa za Vyakula na Nishati

Mfumuko wa Bei ambao haujumuishi vyakula na nishati kwa mwezi Desemba, 2016 umepungua kidogo hadi asilimia 2.5 kutoka asilimia 2.6 mwezi Novemba, 2016.

Fahirisi inayotumika kukokotoa aina hii ya Mfumuko wa Bei, haijumuishi vyakula vinavyoliwa nyumbani na migahawani, vinywaji baridi, petroli, dizeli, gesi ya kupikia, mafuta ya taa, mkaa, kuni na umeme. Vyakula na bidhaa za nishati vina sifa ya kuwa na bei ambazo hubadilika mara kwa mara, hivyo vikiondolewa kwenye fahirisi ya bidhaa na huduma zote hubakia fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa Watunga Sera.

Kielelezo Namba 1: Mwenendo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei Kutoka Mwezi Desemba, 2015 hadi Desemba, 2016. (Des., 2015 = 100)



Kielelezo Namba 1 hapo juu kinaonesha kuwa, Fahirisi za Bei zimekuwa na mwenendo imara kutoka mwezi Desemba, 2015 hadi mwezi Desemba, 2016. Katika kipindi hicho, Mfumuko wa Bei nao umekuwa na mwenendo imara kutoka asilimia 6.8 mwezi Desemba, 2015 hadi asilimia 5.1 mwezi Desemba, 2016.

MFUMUKO WA BEI WA MWEZI DESEMBA, 2016 KWA KIPIMO CHA MWEZI UMEONGEZKA KWA ASILIMIA 0.7

Mfumuko wa Bei wa mwezi Desemba, 2016 unaopimwa kwa kipimo cha mwezi umeongezeka kwa asilimia 0.7 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 1.1 ilivyokuwa mwezi Novemba, 2016. Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 105.04 mwezi Desemba, 2016 kutoka 104.32 mwezi Novemba, 2016. Kuongezeka kwa Fahirisi za Bei kumechangiwa hasa na kuongezeka kwa bei za baadhi ya bidhaa za vyakula. Baadhi ya bidhaa za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa fahirisi ni pamoja na mahindi kwa asilimia 12.6, unga wa mahindi kwa asilimia 12.2, mtama kwa asilimia 8.9, unga wa

muhogo kwa asilimia 3.5, dengi kwa asilimia 12.5, ndizi za kupika kwa asilimia 4.7 na maharage kwa asilimia 3.3.


THAMANI YA SHILINGI YA TANZANIA MWEZI DESEMBA, 2016 KUTOKA MWEZI DESEMBA, 2015

Thamani ya Shilingi ya Tanzania hupima badiliko la Uwezo wa Shilingi ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma zilezile za mlaji ambazo Shilingi ya Tanzania ingeweza kununua katika vipindi tofauti. Ikiwa Fahirisi za Bei za Taifa zinaongezeka, Uwezo wa Shilingi ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma hupungua.

Uwezo wa Shilingi 100 ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma umefikia Shilingi 95 na senti 20 mwezi Desemba, 2016 ikilinganishwa na Shilingi 95 na senti 98 ilivyokuwa mwezi Novemba, 2015.

MIENENDO YA BEI

Kielelezo Namba 2: Mienendo ya Bei kwa Makundi Mbalimbali ya Fahirisi za Bei Kutoka Mwezi Desemba, 2015 hadi Desemba, 2016. (Des., 2015 = 100)



Kielelezo Namba 2 hapo juu kinaonesha mienendo ya bei kwa makundi mbalimbali ya Fahirisi za Bei kuanzia mwezi Desemba, 2015 hadi mwezi Desemba, 2016. Kwa wastani, Fahirisi za nishati na mafuta na Fahirisi za vyakula na vinywaji baridi zimekuwa na mwenendo wa juu kwa kipindi chote zikilinganishwa na fahirisi nyingine. Kundi la nishati na mafuta limeonesha pia kuwa na mwenendo wa fahirisi usio imara ikilinganishwa na makundi mengine kwa kipindi husika. Fahirisi za bidhaa zisizo za chakula na fahirisi za bidhaa zisizo jumuisha chakula pamoja na nishati zimeonesha mwenendo wa bei ulio imara.

**Jedwali Namba 2: Mwenendo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei
Kutoka Mwezi Januari hadi Desemba, 2016. (Septemba 2010 = 100)**

Mwezi	Fahirisi za Bei za Taifa	Mfumuko wa Bei wa Taifa (%)	Mfumuko wa Bei wa Bidhaa za Vyakula (%)	Mfumuko wa Bei wa Bidhaa Zisizo za Vyakula (%)	Mfumuko wa Bei ambao Haujumuishi Vyakula na Nishati (%)
Jan-16	100.71	6.5	10.3	2.0	2.4
Feb-16	101.44	5.6	9.1	1.9	2.5
Mar-16	101.93	5.4	8.0	3.0	2.8
Apr-16	102.46	5.1	7.3	3.5	3.0
May-16	103.00	5.2	7.2	3.8	3.0
Jun-16	103.47	5.5	8.3	3.6	3.0
Jul-16	103.50	5.1	7.8	3.2	2.6
Aug-16	103.28	4.9	7.0	3.0	2.6
Sep-16	103.05	4.5	6.1	2.7	2.4
Oct-16	103.17	4.5	6.0	2.9	2.4
Nov-16	104.32	4.8	6.4	3.8	2.6
Dec-16	105.04	5.0	7.4	3.8	2.5
Wastani 2016	102.95	5.2	7.6	3.1	2.6
Wastani 2015	97.89	5.6	8.6	1.8	2.3

Jedwali namba 2 linaonesha mwenendo wa bei za bidhaa na huduma za jamii na Mfumuko wa Bei kutoka mwezi Januari hadi Desemba, 2016. kwa ujumla, mwenendo wa bei za bidhaa na huduma za jamii ulikuwa imara kwa kipindi chote cha mwaka kutoka Januari hadi Desemba, 2016. Fahirisi za Bei ziliongezeka kutoka 100.71 mwezi Januari, 2016 hadi 105.04 mwezi Desemba, 2016. Mwenendo huu wa bei za bidhaa ulisababisha kuwe na Mfumuko wa Bei ulio imara kwa kipindi chote cha mwaka ambapo, kiwango kidogo kabisa cha Mfumumuko wa Bei kilikuwa asilimia 4.5 kwa miezi ya Septemba na Oktoba, 2016 na kiwango cha juu kabisa kilikuwa asilimia 6.5 mwezi Januari, 2016.

Wastani wa Mfumuko wa Bei wa Taifa (kutoka Januari hadi Desemba, 2016) ulipungua hadi asilimia 5.2 mwaka 2016 kutoka wastani wa asilimia 5.6 ilivyokuwa mwaka 2015 (kutoka Januari hadi Desemba, 2015). Kupungua kwa wastani wa Mfumuko wa Bei wa Taifa kulichangiwa hasa na kupungua kwa kasi ya kupanda kwa bei za bidhaa za vyakula. Wastani wa Mfumuko wa Bei wa bidhaa za vyakula ulipungua hadi asilimia 7.6 mwaka 2016 kutoka asilimia 8.6 mwaka 2015. Kwa upande mwingine, wastani wa Mfumuko wa Bei wa bidhaa zisizo za vyakula kwa mwaka 2016 uliongezeka hadi asilimia 3.1 kutoka asilimia 1.8 ilivyokuwa mwaka 2015. Wastani wa Mfumuko wa Bei ambao haujumuishi vyakula na nishati nao uliongezeka kidogo hadi asilimia 2.6 mwaka 2016 kutoka asilimia 2.3 mwaka 2015.

Jedwali Namba 3: Shajala ya Fahirisi za Bei za Taifa kwa Miezi Ijayo

Fahirisi za Bei za Taifa	Tarehe ya Toleo
Januari, 2017	08 Februari, 2016
Februari, 2017	08 Machi, 2016
Machi, 2017	10 Aprili, 2017

**Mawasiliano: Mkurugenzi Mkuu,
Ofisi ya Taifa ya Takwimu**